**336/2**
**KISWAHILI**
Karatasi
ya Pili
**Paper 2**
August 2024
**Saa mbili**

**ENTEBBE JOINT EXAMNATION BUREAU**

**Uganda Lower Secondary Certificate of Education**

**KISWAHILI**

Karatasi ya Pili

Ufahamu na uchambuzi wa fasihi

**Saa mbili**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

*Karatasi hii ina sehemu*; **mbili; A***na* **B.**

*Maswali yote ni ya* **lazima**.

*Majibu yote yaandikwe kwenye karatasi uliyopewa.*

*Swali la ziada halitasahihishwa.*

*Nadhifisha mwandiko wako.*

## SEHEMU A

## UFAHAMU

**1. Soma taarifa hii kisha ujibu maswali atakayofuata.**

### LUGHA YA KISWAHILI

Lugha ya Kiswahili ndio lugha muhimu katika eneo lote la Afrika Mashariki na Kati. Hiini kwa sababu lugha hii ina nafasi ya kipekee katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda.Katika nchi hizi, Kiswahili ni Lugha ya Taifa. Pia, wananchi wengi wa Afrika Masharikiwanaelewana na huitumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao, hivyo kuipa lughahii nafasi ya kipekee katika mambo muhimu kama utamaduni, siasa na uchumi.

Wataalamu wengi wa masuala ya utamaduni wanakubaliana kwamba kwa kiasi kikubwa,lugha ni kielelezo cha utamaduni. Ukweli huo hujidhihirisha katika lugha yenyewe.Ukichunguzakwa makini lugha yoyote, utagundua kwamba ina vipengele mbalimbalivya utamaduni wawasemaji wa lugha hiyo ambavyo vinajitokeza ndani mwake.

Vilevile, nafasi iliyonayo Kiswahili katika masuala ya siasa ni jambo lisilohitaji kupigiwangoma. Tangu enzi za wakoloni. Lugha ya Kiswahili ilitumika kama chombo muhimuchakuunganisha watu na kuleta umoja. Harakati nyingi ziliendeshwa kwa Kiswahili.Kwa kuwa Kiswahili ndio lugha itumiwayo na watu wengi katika Afrika Masharikikuleta uelewano, basi ndio lugha wanasiasa hutumia katika mikutano yao.

Aidha, Kiswahili ndio lugha pekee ambayo inazungumzwa zaidi dhidi ya lugha nyinginekatika maeneo ya afrika Mashariki, Kati na Kusini ambapo zipo lugha nyingi.Katika ukuaji wa uchumi, Kiswahili ni muhimu vilevile. Lugha ambayo inafahamika kwawatu wengi ndio ifaayo kutumiwa katika mawasiliano ya kibiashara. Tangu zamani,wananchi wa Afrika Mashariki wamekuwa wakiitumia lugha hii katika shughuli zao zakibiashara. Kiswahili bila wasiwasi wowote. Pia, Mtanzania anaweza kuingia Kenya,vijijini, akaendesha shughuli zake za kibiashara bila taabu ya kumtafuta mkalimani. Halihii pia inajiakisi katika jamhuri ya demokrasia ya Kongo, Malawi, Ngazija (Comoros), Burundi na Rwanda.

Siku hizi, Kiswahili kinatumika katika idhaa za nchi za ulimwengu kama vile Uchina, Afrika Kusini, Urusi, Ujapani, Ujerumani, India na nyingine ambapo Kiswahilikimepewa nafasi. Aidha, vyuo vikuu mashuhuri duniani kama vya nchini Marekani, Uingereza, Ujapani, Korea, Urusi, Uchina na kwingine sasa vinafundisha Kiswahili.Isisahaulike kuwa Kiswahili ni lugha mojawapo rasmi ya Umoja wa Afrika.

Kiswahili kinaendelea kukua kila kukicha na kilichobaki ni kwa wakereketwa waKiswahili kuendelea kukieneza na kukipangia mikakati mingi inayoweza kusaidiakukiendeleza ili kiweze kusambaa kwa mapana marefu.

**Maswali;**

(a) Kwa nini mwandishi anasema kuwa nafasi ya Kiswahili katika siasa "haifai kupigiwangoma"?

(b) Ni nini inayoonyesha kwamba Kiswahili sasa imekuwa lugha ya Kimataifa?

(c) Unafikiri Lugha ya Kiswahili ina umuhimu gani?

(d) Kiswahili hapa Uganda hakijashika mizizi iwezekanavyo, unadhani serikali ya Uganda inafaa kufanya nini ili lugha ya Kiswahili kusambaa vizuri nchini nzima?

## SEHEMU B

## UCHAMBUZI WA FASIHI

**2. Soma dondoo hili kisha ujibu maswali yatakayofuata.**

*(Ndani ya kilabu ya pombe. Chupa za pombe zimepangwa katika rafu. Jengo limeandikwa "Maskini Hana Raha" na watu wanaendelea kufurahia maisha yao kwa vinywaji aina aina vikisafirishwa na mziki ulionyooka. Kuna mziki wa 'Money is no a problem but a problem is how you use it').*

**Meneja:** *(Akiwa na uso wenye furaha)* Kila mtu atume kinywaji kulingana na hiari yake na pocket money yake. Hakuna 'nipe deni' au 'nitalipa kesho hapa'.

**Liyongo:** *(Anaonekana amelewa kabisa. Hana mbele wala nyuma. Anamwangalia meneja kwa hasira. Anaongea kwa kuboboja)* Mshenzi wee!
Po..keee...tii..... po....keee...tii.. mo..ne..y ni maaa....maa...ko fala wee!

**Meneja:** *(Anakenua macho huku anamwendea Liyongo kwa hasira)* Wewe maskini unatapika nini? Wewe mteja wa aina gani? Umefika hapa saa mbili zilizopita na sasa hujamaliza kunywa chupa moja. Huna pesa. Ona unakunywa *Smirnoff* kama mwanamke.

**Liyongo:** *(Anajaribu kubanduka kwenye plastiki chair na anashindwa. Pakiti ya sigara aina ya Rali inadondoka chini na kapakiti kadogo kenye kuandikwa 'kuber')* Meneja wacha ujii...ngaa... apa! Sisi matajiri

tunaleee...ta pesa na wewe uko apa kwa umaskini wako. Sasa ona hii bar yako. Umeshindwa kuleta mabinti.

**Meneja:** *(Anaangua kicheko cha kejeli ha! ha! ha!. Anaondoka kuelekea chumba kingine. Anasikika akiongea na watu)* Mariana uko wapi? Naamini umejipiga perfume yako ile ya gift of Zanzibar.
Hebu twende. Kuna mteja anataka kuonja utamu wa maisha.

**Mariana:** *(Amefuatana na Meneja. Anasimama mbele ya Liyongo)* Meneja umepoteza muda wangu. Huyu maskini huyu mifuko yake ni jangwa kabisa.

**Liyongo:** *(Anaruka maramoja kwa hasira. Mkono kwenye mfuko wa suruali yake na anatoa kifurushi cha pesa za noti 50,000 na 20,000)* Huyu ni mama yako fuuu...mbaaa...fu. Kuja apa. Shika na vidole vyako uone kama ni karatasi wee fala.

**Mariana:** *(Kwa hamu na nguvu nyingi. Anyakua pesa zote)* Sasa wewe ni tajiri kweli. Njoo ushike, ubusu, uchuchuze matiti yangu na uufanyie mwili wangu chochote unachotaka. Bibilia inasema wazi eti kila mtu atakula kwa jasho lake......... basi tuingie chumbani nikuonyeshe utamu wa maisha.

**Liyongo:** *(Hawezi kusimama wima. Taa za rangi aina aina zinazidi kumulika. Anampiga kiganja kwenye makalio, anambusu)* Mapenzi hayana macho! *(Watu wote wanacheka)* Wewe ni mavuno kabisa. Hizo si pesa.
Niko na pesa zaidi mimi. Nikupe PIN uende mwenyewe mobile money.

**Mariana:** *(Akiita kwa sauti nyororo)* Meneja naomba nipate funguo. Hebu nimpeleke customer wangu machinjioni.
*(Wote kwa pamoja wanaangua kicheko kwa! kwa! kwa!. Mariana na Liyongo wanaingia mlango mwingine na kuufunga puu!)*

**Mariana:** *(Kwa furaha. Amejifunika Kanga. Anaelekea chumba namba 20 akiongea peke yake)* Mwili wangu ni mali yangu na kila mtu ni mteja wangu. Anayepinga aende kwa mama yake.

**Liyongo:** *(Anatabasamu huku anavaa shati lake. Zipu ya suruali imefunguliwa na mpini unasalimu watu. Mkanda unaning'inia. Anaongea peke yake)* Hii pesa haijakufa bure. Dada huyu amelowa rovu rovu. Nimempiga bila helmet. Pesa yangu nimeitumia yote na kupata utamu wa maisha. Mungu alimpa rasilimali binti huyu.

**Askari:** *(Kwa hasira anashika hapa na pale. Anaokota pistol yake)* Kijana

maneno yako yametuchokoza akili. Sisi tuna mwili pia Tuachie shida zetu tuteremshe machozi ya Simba tumboni.

*(Askari anaangalia kwa hasira zaidi. Anarusha chupa ya BELL na sigara ya SPORTSMAN.Anapiga risasi tu! tu! tu! tu! kumlenga Liyongo. Kila mtu anatawanyika kwa dira yake).*

**Maswali:**

(a) Fafanua mandhari ya onyesho hili.

(b) Jadili maudhui yanayodhihirishwa katika dondoo hili.

(ch) Onyesha mambo ambayo hayakupendezi kulingana na dondoo hili.

(d) Eleza matatizo ya kutumia vileo kulingana na dondoo hili.

(e) Chambua mbinu ambazo zimetumiwa na mwandishi wa dondoo hili.

(f) Unafikiri Vijana ambao wana tabia kama vile Liyongo na Mariana wanaweza kupata shida zipi?

(g) Kulingana na tabia za Liyongo, Mariana na Askari, vijana wa siku hizi unawapa ushauri gani?



**MWISHO**